HOTUBA YA KAIMU MTENDAJI MKUU KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI, TAREHE 28 APRILI, 2019

VIWANJA VYA BUSTANI YA JIJI- MKOANI MBEYA

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Nchi-Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mh. **Jenister Joakim Mhagama (Mbunge)** na wageni wote waalikwa tuliojumuika hapa.

Asalam alekum…… Tumsifu Yesu Kristu…… Bwana Yesu Asifiwe….

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya na kutukutanisha hapa leo kwenye kilele cha maadhimisho ya siku hii ya Usalama na Afya mahali pa kazi duniani. Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi pamoja na majukumu mazito uliyonayo hasa katika kipindi hiki cha bunge, lakini kwakutambua na kuthamini shughuli hii umekubali kuwa nasi leo katika maadhimisho haya, nakushukuru sana.

Vilevile, naomba niwashukuru wadau wetu wa utatu, TUCTA na ATE bila kuwasahau Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana nasi kwa karibu katika maandalizi ya maadhimisho haya. Kwa kipekee kabisa naomba nimshukuru Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani kanda ya Afrika Mashariki, Bwana Wellington Chibebe kwa kutambua kuwa katika kanda anayoisimamia, yaani kanda ya Afrika Mashariki, Tanzania ina mfumo mzuri wa Usimamizi wa masuala Usalama na Afya za wafanyakazi katika sehemu za kazi ukilinganisha na nchi nyingine katika eneo lake.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kazi yangu hapa ni kukutambulisha wageni mbali mbali waliopata fursa ya kujumuika nasi katika maadhimisho haya yanayofanyika kitaifa hapa mkoani Mbeya.

Hivyo, naomba utambue uwepo wa wageni wafuatao;

Mh. Antony Mavunde Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,

Mh. Stella Ikupa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,

Mh. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya,
Mh. Paul Ntimika - Mkuu wa Wilaya Mbeya Mjini,

Ndugu Andrew Massawe Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,

Dr.Adlehem Meru, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya OSHA,

Ndugu Tumaini Peter Nyamhokya Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

Dr. Yahaya Msigwa – Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

Ndugu Jealous G. Chirove, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa ILO Kanda ya Afrika Mashariki.

Ndugu Danisora Tandasi, Mwakilishi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Ndugu Wakurugenzi wote, kutoka ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Ajira,Vijana na watu wenye Ulemavu na

Wakurugenzi na Watendaji wote wa OSHA,

Watendaji wote wa Serikali walioko hapa,

Viongozi wa vyama vya wafanyakazi, wakiwemo wenyeviti na makatibu wakuu,

Wakuu wa Taasisi Mbalimbali,

Ndugu wanahabari,

Washiriki wote wa maadhimisho haya,

Mabibi na Mabwana.

ITIFAKI IMEZINGATIWA

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, hao ni baadhi ya viongozi walioweza kufika hapa kushirikiana nasi katika maadhimisho haya ya siku ya Usalama na afya Duniani. KARIBUNI SANA

Pamoja na kazi hii ndogo ya kukutambulisha wageni tulioungana nao leo, napenda kueleza kwa kifupi chimbuko la maadhimisho haya na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi maadhimisho haya ambayo hufanyika kila mwaka, huandaliwa na OSHA kwa niaba ya serikali kwa kushirikiana na wadau wa utatu(tripartite) ambao ni Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambapo kupitia vikao mbalimbali hujadili namna ya kuiadhimisha siku hii. Ujumbe wa mwaka huu ni: **Usalama na Afya na mustakabali wa kazi kuelekea uchumi wa viwanda.**

Mhe. Mgeni Rasmi, chimbuko la maadhimisho haya yalianza kwa mara ya kwanza tarehe 28 Aprili 1996 huko katika Jiji la New York nchini Marekani. Kuanzia wakati huo, maadhimisho haya yalikuwa yakiadhimishwa kila mwaka na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Duniani chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa. Lengo kubwa la maadhimisho haya ilikuwa ni kuwakumbuka wafanyakazi waliokua wanaumia au kupoteza maisha wakiwa katika sehemu za kazi. Ilipofika mwaka 2003, Shirika la kazi Duniani (ILO) likaungana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi katika kuadhimisha siku hiyo. Mwaka uliofuata yaani 2004, ILO likapendekeza kuwa lengo la maadhimisho hayo libadilike. Badala ya kuadhimisha kwa kusikitika, kuhuzunika na kuwasha mishumaa maadhimisho hayo yafanyike kwa kuhamasisha wafanyakazi, waajiri na umma kwa ujumla kufanya juhudi za makusudi kabisa ili kuzuia ajali na vifo miongoni mwa wafanyakazi. Kuanzia wakati huo, kila mwaka ILO kwa kushirikiana na wadau wa utatu wamekuwa wakitoa kauli mbiu tofauti zenye lengo la kuimarisha usalama na afya sehemu za kazi na kuziomba nchi wanachama waanze rasmi kuadhimisha maadhimisho haya. Hapa kwetu Tanzania tumekuwa tufanafanya maadhimisho hayo kwa takribani miaka 16 sasa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi Kwa mwaka huu wadau, wameazimia kutekeleza shughuli mbali mbali zinazolenga kuhamasisha utekelezaji wa

sheria Na.5 ya Mwaka 2003, ya Usalama na Afya mahali pa kazi kwa kufanya yafuatayo:

- kuendelea kufanya kaguzi za kiusalama na kiafya katika sehemu kazi,
- Kufanya mafunzo mbalimbali ya utekelezaji wa sheria tajwa, kama vile uundaji na usimamizi wa Kamati za Usalama na Afya mahali pa kazi.
- Kufanya makongamano ya wataalam wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi
- kuandaa maonesho yanayolenga katika kubadilishana uzoefu wa uzingatiaji wa usalama na afya sehemu mbalimbali za kazi,
- kutoa tuzo kwa waajiri wanaozingatia vyema viwango vya Usalama na Afya, ambao leo hii Mheshimiwa Mgeni Rasmi, utawakabidhi tuzo zao hapa.

Aidha katika maonesho haya washiriki takribani 40 wameshiriki ikilinganishwa na mwaka jana ambapo washiriki 18 tu ndio walioshiriki aidha kwa mwaka huu washiriki 27, wameshiriki katika tuzo ikilingalishwa na washiriki 17 wa mwaka jana ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 100.

Kubwa zaidi **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ni utekelezaji wa agizo lako ulilolitoa la kuhakikisha kuwa tunaifikia sekta isiyo rasmi, ambapo kwa mwaka huu serikali kupitia OSHA imetoa mafunzo ya Usalama na Afya katika sekta ya madini na shughuli nyingine za kiuchumi kwa washiriki wapatao 16,897 wakiwemo 5,672 kutoka katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Songwe, Katavi, Iringa, Njombe na hapa Mbeya ambako jumla ya mafundi katika fani mbali mbali wapatao 3,070, waliweza kupata mafunzo hayo. Vilevile OSHA ilishiriki katika kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyama vya wafanyakazi wapatao 116. Mafunzo haya yalilenga kutoa elimu juu ya namna bora ya kuzuia na kujikinga na athari zinawezoweza kuwapata kutokana na mazingira hatarishi katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, pamoja na makundi hayo tuliyoyafikia kundi ambalo tumelitazama pia kwa jicho la pekee ni watu wenye ulemavu ambao wakati mwingine huwa wanasahaulika katika masuala mbalimbali ikwemo Usalama na Afya mahali pa kazi.Hii ni kutokana na ukweli kwamba watu wenye ulemavu wanauwezo wa kufanya kazi aidha kwa kujiajiri ama kuajiriwa, hivyo sisi kama OSHA tumefanya mafunzo maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu wapatao 300 kwenye fani mbalimbali. Ambapo

pamoja na mafunzo hayo walipatiwa vifaa vya kujikinga na vihatarishi ili kuwawezesha kufanya kazi zao kiufanisi.

Mafunzo hayo yote kwa makundi tajwa yamegharamiwa na serikali.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Usalama na Afya mahali pa kazi ni masuala mtambuka kwani yanamgusa kila mmoja wetu katika sekta zote bila kujali kuwa ameajiriwa ama amejiajiri.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, hakuna shaka sote tunatambua kwamba mwelekeo wa nchi yetu kwa sasa ni kujenga uchumi wa viwanda, na hivyo katika kuelekea huko ajira nyingi zitazalishwa na watanzania wengi wataajiriwa katika sekta mbalimbali za uzalishaji. Ni dhahiri kwamba maendeleo haya ya uchumi wa viwanda yanaambatana na athari mbalimbali za kiusalama na kiafya, ambazo kama hakuna mkakati madhubuti wa kuzuia athari hizo, nguvu kazi ya taifa itakuwa hatarini. Hivyo, OSHA kama taasisi yenye dhamana ya kusimamia masuala ya Usalama na Afya imejipanga vyema kuhakikisha kuwa athari hizo zina dhibitiwa kwa kufanya yafuatayo:

- Kuongeza uelewa miongoni mwa wadau ambayo hii ndio changamoto kubwa.
- Pamoja na kusimamia kikamilifu Sheria Na.5 ya Mwaka 2003 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.
- Kuendeleza programu maalum zinazolenga kuyafikia makundi mbalimbali ya uzalishaji mali katika sekta isiyo rasmi
- Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa OSHA ili kuendana na mabadiliko tunayoyatarajia.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kwa kuhitimisha ningependa kuwakumbusha Waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia viwango vya usalama na afya vilivyowekwa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, ningependa kutumia fursa hii kuushukuru uongozi wa mkoa wa Mbeya kwa kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho haya. Ni imani yangu kuwa imekuwa ni fursa nzuri kwa wana Mbeya kuweza kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka washiriki wanaotoka katika mikoa mbalimbali kuhusiana na utekelezaji wa sheria ya usalama na afya mahali pa kazi.

Baada ya kusema hayo Mheshimiwa Mgeni Rasmi, naomba nikushukuru tena wewe binafsi na viongozi wote uliombatana nao, aidha shukrani hizi pia ziwaendee wadau wetu na washiriki wote wa maadhimisho haya.

Kwa niaba ya uongozi mzima wa OSHA tunawatakia maadhimisho mema.

Asanteni kwa kunisikiliza